

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01–10 APRILI, 2018 NA MATARAJIO YA MVUA KWA SIKU KUMI ZA PILI ZA MWEZI APRILI (11– 20 APRILI, 2018)

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01–10 APRILI, 2018

Kati ya tarehe 01-10 mwezi Aprili 2018, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) uliendelea kuwepo kati ya maeneo kaskazini na kusini mwa Tanzania. Joto la bahari katika maeneo ya kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani na kusababisha uwepo hafifu wa vimbunga baharini. Upepo ulivuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi hali iliyoashiria kuimarika kwa ukanda wa mvua wa ITCZ.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01–10 APRILI, 2018

Mwenendo wa viashiria vya hali ya hewa hapo juu vinaonyesha uwepowa ukanda wa mvua wa ITCZ ulipelekea vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini na magharibi mwa nchi wakati maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa kusini pamoja na pwani ya kusini vilikuwa na vipindi vichache vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi. Katika kipindi hichi maeneo ya nyanda za juu kaskazini-mashariki na kanda ya kati viliripoti viwango vidogo vya mvua kulinganisha na maeneo mengine ya nchi.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KATIKA SIKU KUMI ZA PILI KWA MWEZI APRILI (10–20 APRILI, 2018)

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA SIKU KUMI ZA PILI ZA APRILI (11–20 APRILI, 2018)

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuendelea kusogea taratibu kuelekea kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hali inayopunguza uwezekano wa kutokea vimbunga katika bahari. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi hususan katika siku tano za mwanzo na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi na baadae kusambaa hadi nchi nzima. Hali ya joto la bahari inaonyesha joto la juu ya Wastani katika maeneo ya ukanda wa Pwani hali inayoashiria kuendelea kwa mvua katika maeneo hayo. Eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupunguza kwa upepo

uvumao kutoka kagharibi hivyo kupunguza mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi hasa kuelekea nusu ya pili ya siku kumi za kati za mwezi Aprili.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA SIKU KUMI ZA PILI ZA MWEZI APRILI (11–20 APRILI, 2018)

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro,): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Imetolewana; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**